USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

SERA YA SHIRIKA LA MAENDELEO YA KIMATAIFA LA MAREKANI (USAID)

# Kuhusu Msaada wa Kibinadamu Unaoongozwa na Wenyeji

JULAI 2024









*JALADA (kuzunguka kuelekea kulia kutoka juu)*: Kwa ufadhili wa USAID/BHA, Shirika la Shafak, shirika la ndani la Syria, lasaidia wanawake walioathiriwa na vita kuanzisha maisha mapya na kukimu mahitaji ya familia zao. *Picha kwa hisani ya Shirika la Shafak.* • Mwenyekiti wa Kamati ya Maji katika Mji wa Naagan, nchini Kenya akagua chanzo cha maji kinachosimamiwa na jumuiya, ambacho kilipangwa na jumuiya hiyo na kuboreshwa kwa usaidizi wa mradi wa I-CREATE unaofadhiliwa na USAID/BHA. *Picha kwa hisani ya Concern Worldwide US.* • Mshirika wa ndani wa USAID/BHA liitwalo Fedecovera, R.L. lashirikisha mtandao wake wa vyama vya ushirika vya wazalishaji wadogo na jumuiya zao nchini Guatemala ili kupunguza hatari ya maafa na kupata nafuu kutokana na majanga, ikiwa ni pamoja na kupitia usaidizi kwa vikundi vya akiba na mikopo vinavyoongozwa na wanawake. *Picha kwa hisani ya Fedecovera, R.L.* • - Mshirika wa ndani wa USAID/BHA liitwalo Shirika la Msalaba Mwekundu la Vietnam (VNRC) lasaidia mtandao wa zaidi ya matawi 60 ya mikoa kote nchini Vietnam ili kuboresha uwezo wao wa kuwa tayari kukabiliana na dharura ili kuokoa maisha katika majanga. *Picha kwa hisani ya VNRC.*

# Yaliyomo

MUHTASARI .......... 2

UTANGULIZI .......... 4

USULI .......... 6

KANUNI ZINAZOTOA MWONGOZO .......... 10

UPEO WA SERA .......... 12

UTUMIAJI WA SERA .......... 15

MAFUNZO .......... 21

HITIMISHO .......... 21

UFAFANUZI MUHIMU .......... 22

MAREJELEO .......... 23

# MUHTASARI

Idadi ya watu wanaohitaji msaada wa kibinadamu duniani kote ndiyo idadi ya juu ukiilinganisha kihistoria kutokana na majanga na athari za mabadiliko ya tabianchi duniani. Kila janga ni la kipekee, linalochagizwa na masuala ya eneo husika na linahitaji kuchukuliwa kwa hatua ya kibinadamu yenye uwajibikaji, inayofaa, na yenye ufanisi — iliyobinafsishwa kulingana na mahitaji ya kipekee ya makundi yaliyoathiriwa. Kulingana na uzoefu wa miaka mingi wa kufanya kazi na vikundi vya eneo husika, shirika la USAID linajua kuwa mashirika na jumuiya za eneo husika zilizo karibu na janga zipo katika nafasi nzuri ya kutambua mahitaji, kuongoza vipaumbele vya kukabiliana na janga na kutathmini na kurekebisha mipango.

Utambuaji wa haja la kuongeza uongozi wa wahusika wenyeji katika uwekaji wa masuala ya kipaumbele, muundo wa mradi, utekelezaji na upimaji wa matokeo na kama sehemu kuu ya dhamira dhabiti ya Shirika ya kuendeleza ujanibishaji, katika mwaka wa 2021 shirika la USAID lilianza kutekeleza mageuzi ya ndani ya Shirika lote kuelekea kuafikia malengo yafuatayo: 1) kuelekeza angalau asilimia 25 ya fedha moja kwa moja kwa wahusika wenyeji ifikapo mwaka wa 2025[1] na 2) kuhakikisha kuwa angalau asilimia 50 ya shughuli zinazofanywa zinaongozwa na wenyeji ifikapo mwaka wa 2030.[2] Ahadi hizi zimeongoza shirika la USAID katika kupanua ushirikiano na wahusika wenyeji, kuwa na mtazamo mpya wa uhusiano na mashirika ya kimataifa na kurekebisha jinsi linavyotekeleza kazi ya kuokoa maisha inayotekelezwa kupitia Ofisi ya Misaada ya Kibinadamu (Bureau for Humanitarian Assistance, BHA). Juhudi hizi za shirika la USAID zinaongozwa na huchangia katika mageuzi ya kimataifa ya kibinadamu kama vile Grand Bargain.[3]

Ili kufanya mageuzi haya yaliyo mahususi kwa suala la utoaji wa msaada wa kibinadamu, shirika la USAID limetayarisha Sera hii inayohusu Shughuli ya Kutoa Msaada wa Kibinadamu Inayoongozwa na Wenyeji (LLHA) ili kushughulikia mipango pamoja na mwendelezo unaojumuisha shughuli za kukabiliana na hali ya dharura, uokoaji wa haraka, ustahimilivu, na shughuli za kupunguza hatari za maafa (DRR). Ingawa nyingi ya kanuni hizi zinaongoza juhudi za msaada wa kibinadamu na maendeleo za shirika la USAID, shirika la USAID limeunda sera hii likiwa na maono mahususi ya kuziweka jumuiya za wenyeji kuwa wahusika wakuu katika kazi ya kibinadamu na kusaidia mfumo wa kibinadamu unaozingatia maamuzi na vipaumbele vinavyohusiana na eneo ambavyo vinawakilisha sauti za makundi yaliyoathirika. Kwa kufanya hivyo, shirika la USAID linaweza kutoa msaada wa kibinadamu wenye uwajibikaji zaidi, unaofaa na ulio na ufanisi iwezekanavyo, huku pia ikijenga ustahimilivu wa jamii na kudhibiti hatari za janga.

1 Ufadhili wa moja kwa moja wa eneo husika hupimwa kama asilimia ya jumla ya fedha za maendeleo na za msaada wa kibinadamu zinazohitajika katika mwaka fulani wa kifedha, bila kujumuisha usaidizi wa serikali ya washirika, mikataba kati ya mashirika, kandarasi za huduma za kibinafsi na mikataba ya Mashirika ya Umma ya Kimataifa (PIO). Sehemu kubwa ya ufadhili wa shirika la USAID/BHA inaelekezwa kwa PIO na, kulingana na ufafanuzi wa Shirika kuhusiana na kipengele cha ufadhili wa moja kwa moja wa eneo husika, haijajumuishwa kama sehemu ya hesabu ya moja kwa moja ya ufadhili wa ndani.

2 Kiashirio cha Mipango Inayoongozwa na Wenyeji hupima asilimia ya shughuli zinazofadhiliwa na shirika la USAID ambapo washirika na/au jumuiya za eneo husika huongoza juhudi za maendeleo au za kibinadamu, ikiwa ni pamoja na uwekaji wa masuala ya kipaumbele, ubunifu, uundaji wa ushirikiano, utekelezaji na ufafanuzi na upimaji wa matokeo, katika mwaka fulani wa kifedha. Kiashirio cha Mipango Inayoongozwa na Wenyeji kinahusu upangaji wa mipango yote inayofadhiliwa na shirika la USAID, ikijumuisha fedha zinazoelekezwa kwa PIO.

3 Grand Bargain ni makubaliano, yaliyozinduliwa wakati wa Mkutano Mkuu wa Kibinadamu wa Dunia mnamo mwezi Mei 2016, kati ya wafadhili wengi na mashirika ya kibinadamu ili kuboresha ufanisi, ubora, na uwajibikaji wa shughuli za kibinadamu, ikiwa ni pamoja na kukuza uongozi wa eneo husika; serikali ya Marekani ni mtia saini mwenza.

Isitoshe, mahitaji changamano ya shughuli za kibinadamu yana changamoto na fursa, mara nyingi zilizo tofauti na mazingira ya maendeleo. Dhamira yenyewe ya utoaji wa msaada wa kibinadamu; muktadha wa janga; haja ya kuchukuliwa kwa hatua za haraka, ambazo mara nyingi huwa ni za kiasi kikubwa; uwezo wa kipekee na unaoweza kutumiwa kwa haraka; na muundo wa mifumo ya kitaifa na kimataifa ya uratibu wa shughuli za kibinadamu unahitaji mbinu tofauti za kuendeleza uongozi wa wenyeji, kupanua ushirikiano wa wenyeji, na kusaidia uwezo wa wenyeji. Isitoshe, mienendo ya utawala, utumiaji wa mashirika ya kimataifa kama washirika wa utekelezaji wanaofanya kazi nao na kupitia mashirika ya eneo husika, na haja ya kushiriki juhudi za kupunguza hatari na usimamizi kati ya wadau ndani ya mazingira ya uendeshaji wa shughuli za kibinadamu ni mambo muhimu ya kuzingatia katika miktadha hii.

Sera ya LLHA inaongozwa na seti nne za kanuni. Kwanza kabisa, Sera ya LLHA inathibitisha kujitolea kwa Shirika kwa kanuni za ubinadamu zinazoongoza shughuli za kibinadamu, kutoegemea upande wowote, kutopendelea na kujitegemea. Pili, kanuni za usawa, ujumuishaji na ufikiaji zinamaanisha kuwa wahusika wote kwenye ushirikiano, ikijumuisha mashirika yanayowakilisha washirika wapya na wasio wa kawaida, huchangia na kupokea manufaa kutoka kwa ushirikiano huu, kama ilivyobainishwa katika Sera ya shirika la USAID ya Kuimarisha Uwezo Wenyeji. Tatu, kanuni za kuwa na uwezo wa kubadilika na umaalum wa muktadha unamaanisha kuwa juhudi za kuinua na kusaidia uongozi wa wenyeji zitaendelea kwa namna tofauti kulingana na mambo mengi ya muktadha. Hatimaye, kanuni ya Kuzuia Madhara inamaanisha kuwa shirika la USAID litafanya jitihada za kuzuia na kupunguza athari mbaya zinazoweza kutokea kutokana na vitendo vyake kwa washirika na vikundi vya wenyeji, ikiwa ni pamoja na watu walio katika mazingira hatarishi kutokana na hali za dharura za kibinadamu.

Sera ya LLHA inabainisha malengo matano yanayounga mkono maono hii. Malengo haya ni pamoja na 1) kuongeza ufikiaji na kiasi cha ufadhili kwa mashirika ya kibinadamu ya eneo husika; 2) kuimarisha uwezo wa shirika la USAID wa kujenga ushirikiano wa kibinadamu; 3) kuongeza uimarishaji wa uwezo, kushiriki uwezo na kujifunza kwa pamoja katika ushirikiano wa masuala ya kibinadamu; 4) kutetea uongozi wa kibinadamu wa wenyeji; na 5) kutumia diplomasia ya masuala ya kibinadamu na uongozi wa sera. Shirika linapotekeleza mageuzi haya, shirika la USAID linajitolea pia kuendelea na mafunzo ambayo yataendeleza msingi wa ushahidi wa usaidizi wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji. Kwa kukusanya na kuchanganua mafunzo yaliyopatikana katika ushirikiano wa kibinadamu unaoendelea na wa zamani, Shirika linaweza kurekebisha na kuboresha jinsi linavyofanikisha maono yaliyobainishwa katika Sera ya LLHA.

Kama mhisani mkubwa zaidi wa shughuli za kibinadamu duniani, shirika la USAID linapania kutumia nafasi yake kushirikiana na wahisani wengine na mashirika mengine ya kibinadamu ili kuharakisha juhudi hizi za mageuzi. Kwa kushirikiana na wahusika wengine katika sekta ya kibinadamu, shirika la USAID linaweza kuendeleza shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu zinazoongozwa na wenyeji na kuboresha maisha ya watu walioathiriwa na janga duniani kote.

# UTANGULIZI

Idadi ya majanga makubwa ya kibinadamu na yanayotokea kwa wakati mmoja duniani ni kubwa kila wakati, huku mabadiliko ya tabianchi yakiongeza ukali na utokeaji wa mara kwa mara wa hatari za asili pamoja na kuzidisha migogoro kutokana na athari yake kwa upatikanaji wa rasilimali. Ufadhili wa sekta ya kibinadamu—pamoja na uwezo wa kiutendaji wa kukabiliana na majanga haya—unashindwa kuendana na kasi. Shirika la USAID linaongozwa na wazo la kibinadamu—kuokoa maisha na kupunguza mateso ya binadamu—ili kuchukua hatua dhidi ya mengi ya majanga haya, huku shirika la USAID/BHA likihudumu kama mratibu mkuu wa serikali kuu ya Marekani (USG) kwa mchakato wa shughuli za kutoa msaada wa kimataifa wakati wa janga. Msaada wa kibinadamu wa shirika la USAID unafikia kwa haraka watu mbalimbali wenye mahitaji ya kipekee, mara nyingi kwa kiwango kikubwa katika majanga yanayotokea kwa haraka na miktadha tata ya janga duniani kote. Kufuatia utokeaji wa janga au katika dharura tata kama vile vita, shirika la USAID linaweza kuwatuma wafanyakazi wataalamu kwa haraka sana, kutumia akiba iliyotengwa tayari ya vifaa muhimu kwa maisha na kutoa huduma za usafirishaji na usafiri ili kufikia maeneo yaliyoathirika wakiwa na msaada wa kuokoa maisha. Shirika la USAID pia linashiriki na kusaidia mifumo ya kitaifa na kimataifa ya uratibu wa shughuli za kibinadamu zilizo muhimu katika upangaji wa hatua za kibinadamu huku likifanya kazi na wahisani wengine, Umoja wa Mataifa (UN), na mashirika mengine husika ya kibinadamu ili kutoa msaada kwa kuzingatia kanuni za kibinadamu kwa wale walio na uhitaji. Katika mazingira haya ya kibinadamu yanayobadilika kila mara, shirika la USAID kwa bidii na mara kwa mara hutafuta njia mpya za kufanya kazi na kushirikiana na wahusika mbalimbali ili kukabiliana na changamoto ambazo hazijawahi kushuhudiwa.

Ushirikiano na wahusika wa eneo husika ni muhimu ili kutoa msaada wa kibinadamu unaowajibika, wenye ufanisi, na ulio bora, pamoja na kusaidia urejeshaji wa haraka kwa hali ya kawaida, kupunguza hatari na ustahimilivu wa jamii. Wahusika wa eneo, ikiwa ni pamoja na vikundi vya kijamii na taasisi za sekta ya kibinafsi, mara nyingi huwa wa kwanza kukabiliana na majanga ya kibinadamu na kuna uwezekano wa kuwa watasalia katika jumuiya zao wakati na baada ya hali ya dharura. Wahusika wa eneo husika wana ujuzi, uhusiano, na utambuzi wa masuala ya kitamaduni na kisiasa ili kubinafsisha na kuweka kipaumbele cha msaada katika eneo husika. Wahusika wa eneo husika mara nyingi wanaweza kufikia watu walioathiriwa haraka zaidi kuliko vikundi vya nje na wanategemea uhusiano uliopo tayari ambao huwezesha ufikiaji wa maeneo yenye migogoro na jumuiya ambazo ni vigumu kufikiwa. Kushirikisha wahusika mbalimbali kama vile wazalishaji, wasambazaji na watoa huduma wa eneo ili kutafuta bidhaa na huduma ili kushughulikia mahitaji ya kibinadamu kunaweza kuleta matokeo mazuri kwa watu walioathirika na kwa masoko ya eneo husika. Hatimaye, kwa kuzingatia miaka ya uzoefu, shirika la USAID linatambua kuwa kuheshimu uamuzi wa kujitegemea na kuunga mkono ushiriki kamili wa wahusika wa eneo husika—ikiwa ni pamoja na mashirika ya kidini na yale yanayoongozwa na makundi yaliyotengwa kihistoria[4] na makundi yaliyo hatarini—katika miktadha ya kibinadamu ni mbinu bora zaidi inayoweza kusababisha kuongeza ufikiaji wa jumuiya kwa na umiliki wa matokeo ya hatua inayochukuliwa.

4 Watu waliotengwa kihistoria na walio na uwakilishi mdogo wanaweza kujumuisha, lakini sio tu, kaya maskini na maskini zaidi; wanawake na wasichana, pamoja na wajawazito au wanawake wanaonyonyesha; watu wenye ulemavu; watu wenye matatizo ya kiafya; wakimbizi na watu wengine waliohamishwa; wahamiaji; Wazawa; watoto na familia zao; vijana; watu wazee; makundi madogo ya kidini; makundi ya kikabila na ya rangi; watu wa tabaka la chini; watu walio na mahitaji ya afya ya akili ambayo hayajatimizwa; watu wa tabaka tofauti za kiuchumi na walio na maoni tofauti ya kisiasa; na watu wa kundi la LGBTQI+.

Shirika la USAID limewekeza katika suala la uwezo wa uongozi, uendeshaji, upangaji na uwezo wa kiufundi wa washirika wa eneo husika duniani kote kwa miongo kadhaa. Uwekezaji huu wa uboreshaji wa utayari wa kukabiliana na janga na uwezo wa kuchukua hatua umeunda mpango endelevu wa mafunzo na mifumo ya hali ya juu ya kukabiliana na hali ya dharura katika nchi nyingi. Isitoshe, shirika la USAID limeshiriki kwa kiasi kikubwa katika juhudi za kimataifa za mageuzi ya kibinadamu, ikiwa ni pamoja na Mkutano wa Kilele wa Kibinadamu ulioandaliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) mnamo 2016 na matokeo ya makubaliano ya Grand Bargain, ambayo hatimaye yaliongoza wahusika katika mfumo wa kimataifa wa kibinadamu kukumbatia ujanibishaji kama mageuzi muhimu. Uzoefu huu wa muda mrefu sasa unatumika kama msingi wa kupanua mipango iliyofanikiwa na kuanzisha njia mpya za kufanya kazi kwa pamoja.

Shirika la USAID linatambua haja ya kubadilisha jinsi linavyopanga, na masharti yake pia. Hii inamaanisha kurahisisha na kusasisha sera, michakato na mifumo yetu ili kufanya ufadhili uwe wa kufikiwa zaidi, wenye usawa, na unaoweza kudhibitiwa, huku ukipunguza pia mizigo ya usimamizi. Ili kufikia hili, shirika la USAID linakuza ushirikiano wa ndani wenye usawa na unaojumuisha watu wote na kufanya kazi kuhamisha maamuzi kwa uongozi na uwezo wa eneo, inapofaa. Mchakato huu wa muda mrefu lakini wenye umuhimu wa sasa wa mabadiliko ya utamaduni unajumuisha kutambua na kukubali kuwepo kwa tofauti za nguvu ; kurekebisha juhudi za mashauriano na upangaji za Shirika ili kuhakikisha kuwa zinalenga taasisi wakilishi za eneo husika; na kurekodi na kujifunza kutoka kwa mipango ya misaada ya kibinadamu yaliyo ya ubunifu na inayoongozwa na wenyeji ili kuboresha ufaafu, ufanisi, athari na uendelevu wa kazi ya shirika la USAID.

Ili kuharakisha mchakato wa kuhamisha rasilimali zaidi kwa jumuiya za wenyeji, shirika la USAID linaendesha maendeleo na shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji. Tangu 2021, shirika la USAID limetoa Sera yake ya kwanza ya Uimarishaji wa Uwezo wa Wenyeji; limesasisha Taarifa ya Kiwango cha Hatari ambacho Linaweza Kukubali; limebuni njia mpya ya kufuatilia jinsi shirika la USAID linavyotoa kipaumbele kwa uongozi wa wenyeji kwa mipango yake; limesaidia utoaji wa mafunzo ya hali ya juu ya Shirika ili kujumuisha ujanibishaji katika mzunguko wa mpango; limerekebisha na kutoa Mkakati wa Ununuaji na Utoaji wa Msaada to engage a more diverse set of partners; and launched WorkWithUSAID.gov, tovuti ya mtandaoni inaotoa taarifa rahisi na zinazoweza kufikiwa katika lugha nyingi kuhusu kushirikiana na shirika la USAID. Ili kupiga hatua katika kufikia malengo haya, shirika la USAID lilianzisha msururu mabadiliko ya tabia ya ndani ya shirika, mchakato wa sera na mabadiliko ya mfumo—yanaorejelewa kwa pamoja kama ujanibishaji—ili kupanua uwezo wa Shirika wa kusaidia kwa kiasi kikubwa mipango ya maendeleo na utoaji wa misaada ya kibinadamu inayoongozwa na wenyeji zaidi. Kama ilivyorejelewa hapo awali, Shirika liliweka pia malengo ya kuelekeza angalau asilimia 25 ya fedha moja kwa moja kwa wahusika wa eneo ifikapo mwaka wa 2025 na kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa angalau asilimia 50 ya shughuli zinaongozwa na wenyeji ifikapo mwaka wa 2030. Lengo la asilimia 25 ni lengo la Shirika nzima, na malengo ya ndani yanatofautiana katika Misheni za shirika la USAID na Vitengo vya Uendeshaji vya Washington.

Kama sehemu ya mbinu ya Shirika ya ujanibishaji, shirika la USAID limebuni Sera hii ya LLHA ili kueleza mbinu mahususi za kuendeleza ujanibishaji katika miktadha ya kibinadamu. Maono na malengo ya Sera ya LLHA ni kilele cha mchakato wa mashauriano wa miaka miwili na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya shirika, ikijumuisha ushirikishi wa kimakusudi na wahusika wenyeji na mashirika yanayotoa msaada wa kibinadamu.

# USULI

## Ujanibishaji katika Muktadha wa Utoaji wa Msaada wa Kibinadamu

Mahitaji ya shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu yanatoa changamoto na fursa kwa shirika la USAID, ambazo mara nyingi zinatofautiana na mazingira ya maendeleo, kwa kuwa Shirika linajanibisha shughuli, michakato na mifumo yake katika kuunga mkono utoaji wa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji:

- **Dhamira ya Msaada wa Kibinadamu:** Msaada wa kibinadamu umejikita katika kanuni za kibinadamu za ubinadamu, kutoegemea upande wowote, kutopendelea na kuwa huru. Msaada wa kibinadamu unaojikita kwenye kanuni huzuia na kupunguza mateso bila upendeleo au ubaguzi kwa misingi ya rangi, kabila, dini, jinsia au usuli. Katika miktadha ya janga, uzingatiaji wa kanuni hizi huwezesha wahusika wa kutoa misaada ya kibinadamu kupata ufikiaji wa maeneo yaliyoathiriwa na janga, kubaini mahitaji, na kukubalika na kuwasilisha msaada kwa vikundi vilivyo hatarini zaidi, na pia kulinda usalama na ulinzi wa watu wa eneo hilo na wafanyakazi wa kutoa misaada. Ni muhimu kuwa washirika wa kutoa misaada ya kibinadamu wa shirika la USAID, ikiwa ni pamoja na mashirika ya wenyeji na ya kitaifa yanayojishughulisha na uchukuaji wa hatua za kibinadamu, kutoa msaada kulingana na kanuni za kibinadamu.

- **Kasi na Kiwango cha Hatua Inayochukuliwa:** Hali za dharura zinazotokea kwa haraka na mahitaji yanayojitokeza katika majanga yanayoendelea huhitaji Shirika na washirika wake kuchukua hatua haraka, kwa ufanisi, na mara nyingi kwa kiwango kikubwa ili kukidhi mahitaji ya kibinadamu kwa njia inayojikita kwenye kanuni. Ingawa kujenga ushirikiano mpya wa ufadhili wakati wa janga kunaweza kuwa changamoto, ni muhimu kwa shirika la USAID kujumuisha maoni na juhudi za wenyeji katika uchanganuzi na kushirikiana na mashirika ya eneo husika na jumuiya zilizoathirika katika kupanga hatua zitakazochukuliwa. Uwekezaji katika kujitayarisha kwa ajili ya kukabiliana na janga kabla yax kutokea kunaweza kusaidia kutambua na kusaidia wahusika mbalimbali wenyeji ambao shirika la USAID linaweza kushirikiana nao kwa ufanisi katika kuchukua hatua wakati wa hali ya dharura kwa siku zijazo.

- **Mahitaji ya Kipekee ya Uwezo:** Kupeleka msaada wa kibinadamu mara nyingi kunahitaji uwezo thabiti wa vifaa na uendeshaji ili kufikia maeneo yaliyoathirika kwa ajili ya kutoa msaada ulio muhimu katika kuokoa maisha. Washirika wengi wa eneo husika wa shirika la USAID "wana majukumu mawili," wanatekeleza shughuli za maendeleo au kufanya kazi kwenye Muunganisho (Nexus) wa kutoa Msaada wa Kibinadamu-Maendeleo-Amani (HDP) nje ya mazingira ya hali ya dharura (Humanitarian-Development-Peace ,HDP). Katika hali nyingi, washirika wa eneo wanalazimika waelekeze wafanyakazi na rasilimali kutoka kwa miradi yao ya hali thabiti na wanaweza kuwa na akiba ndogo ya vifaa vya kutoa msaada wa kibinadamu vilivyowekwa tayari, uwezo wa usafirishaji au kuongeza wafanyakazi ili kukabiliana na janga. Hata hivyo, kwa kuzingatia uwepo wa wahusika wa eneo husika, mahusiano, na uelewa wa kina wa mienendo ya eneo husika, ushirikiano wa shirika la USAID na wahusika wa eneo husika ni muhimu kwa shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu zinazojikita kwenye kanuni, na zinaoongozwa na wenyeji. Kwa hivyo, kuimarisha uwezo wa kuchukua hatua za usafirishaji, kiutendaji na wa ushirika ni muhimu ili kusaidia uwezo wa wahusika wa eneo kuchukua hatua wakati wa majanga.

- **Miundo ya Uratibu wa Kutoa Misaada ya Kibinadamu:** Timu za Nchi Husika za Kutoa Msaada wa Kibinadamu (HCTs), makundi ya kibinadamu, mifumo ya kitaifa ya kuchukua hatua wakati wa janga na miundo mingine ya uratibu na uwekaji sera huongoza hatua zinazochukuliwa na jamii ya kimataifa

wakati wa majanga ya kibinadamu, lakini mara nyingi sana, mashirika ya eneo hayajumuishwi katika mifumo hii rasmi.[5] Viongozi na mashirika ya eneo yanaweza kutoa mitazamo mbalimbali na ujuzi wa jumuiya unaohitajika ili kuboresha ufanisi wa mikutano hii katika kukidhi mahitaji ya kipekee ya makundi mbalimbali na kuelewa vyema taratibu zinazokubalika na jamii ambazo zinaweza kuchangia katika kupata suluhu thabiti zaidi.

- **Vyanzo vya Ufadhili wa Msaada wa Kibinadamu:** Mifumo ya ufadhili wa msaada wa kibinadamu iliyoanzishwa, kama vile fedha zilizokusanywa katika nchi husika, Hazina Kuu ya Kukabiliana na Dharura, na mbinu zingine za kukabiliana na dharura hutoa fursa kwa mashirika ya ndani kupata rasilimali kwa haraka. Hata hivyo, hatua ya kufikia aina za jadi za ufadhili wa wahisani inaweza kuwa ngumu na inayochukua muda, hasa kwa wale wanaotafuta msaada wa moja kwa moja kwa mara ya kwanza.

## Mienendo ya Nguvu Inaathiri na Inaathiriwa na Hatua za Kibinadamu Zinazochukuliwa

Tofauti za nguvu zingali katika mfumo wa sasa wa kutoa msaada wa kibinadamu kati ya wahisani, washirika wa kimataifa wa utekelezaji na mashirika ya eneo, na vilevile kati ya watu walioathirika na majirani. Uamuzi kuhusu shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu mara nyingi hufanyika mbali na watu na jumuiya zilizoathirika. Miundo ya uratibu wa kutoa misaada ya kibinadamu inaweza pia kuiongeza au kubadilisha tofauti za nguvu zilizopo, kwani wahusika wenyeji mara nyingi hawawezi kushiriki katika vikao vya kufanya maamuzi kwa sababu ya vizuizi vya lugha au ukosefu wa ufikiaji wa mikutano ya uratibu. Katika janga la kibinadamu, haja ya kuchukua hatua ya haraka, ya kuokoa maisha inaweza kuwafanya wahisani na mashirika ya kimataifa kugeukia mashirika yanayojulikana yenye rekodi ya kutekeleza hatua za haraka kwa kiwango kikubwa. Isitoshe, uwekezaji katika mchakato wa kujenga uhusiano wa muda mrefu na ujuzi wa kubadilishana uwezo wa kufanya jambo, kujenga ujuzi, na kuweka kipaumbele katika kujifunza kwa pamoja na mashirika ya wenyeji kunaweza kutatizwa na uzingatiaji wa malengo ya muda mfupi na kipindi cha muda mfupi ambacho mradi utachukua ambao unalenga kushughulikia mahitaji muhimu ya papo hapo, ya kipindi cha muda mfupi. Kujitolea kwa shirika la USAID ya kukubaliana na shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji ni utambuzi wa wazi kuwa jamii zina haki ya kufanya maamuzi muhimu kuhusu maisha yao na kuwa muktadha na uchanganuzi wa eneo ni muhimu katika kuamua nani wa kushirikiana naye katika mipangilio ya kukabiliana na janga.

Sera ya LLHA inakuza ufanyaji wa maamuzi katika ngazi ya kitaifa na kikanda ambayo yanategemea michango kutoka kwa wahusika wenyeji, desturi na mifumo, pamoja na makundi yaliyoathirika, ikiwa ni pamoja na wanawake na makundi yaliyotengwa kihistoria kama vile watu wenye ulemavu, makundi madogo ya kidini na kikabila, watu wa kundi la LGBTQI+ na vijana. Mienendo ya nguvu ndani ya jumuiya za wenyeji inaweza kuathiri utayarishaji wa mpango wa kutoa msaada wa kibanadimu, kwa sababu jumuiya hazifanani na mahitaji yao vilevile hayafanani. Kuna miundo ya nguvu na mipangilio ya kijamii iliyopo ndani ya jumuiya zote, pamoja na upendeleo na ufikiaji usio na usawa wa rasilimali na fursa. Kwa sababu hizi, Upangaji Salama wa Mpango,[6] ambao ni mchakato wa kujumuisha kanuni za usalama katika mipango yote ya kutoa msaada wa kibinadamu ili kukuza usalama na utu, ufikiaji mzuri, uwajibikaji na ushiriki na uwezeshaji, ni kipengele muhimu kwa shughuli zote za washirika wanaotoa msaada wa kibinadamu, uendeshaji na sekta. Hii inahakikisha kuwa makundi yaliyotengwa kihistoria na yaliyo kwenye hatari ndani ya jumuiya zilizoathiriwa yanaweza pia kushiriki kikamilifu, kutoa maoni ya vipaumbele na wasiwasi wao na hatimaye kupata msaada ulio salama na wa heshima.

5 Muundo wa kimataifa wa uratibu wa utoaji wa msaada wa kibinadamu (unajulikana pia kama "usanifu wa kibinadamu") umeundwa ili kuimarisha utabiri, uwajibikaji, na ushirikiano katika mipangilio ya kukabiliana na majanga. HCT ni jukwaa la kufanya maamuzi la mashirika ya kibinadamu (ya Umoja wa Mataifa na yasiyo ya Umoja wa Mataifa) ambayo hutoa mwongozo wa kimkakati na sera kwa ujumla juu ya hatua za kibinadamu katika ngazi ya nchi; makundi ya misaada ya kibinadamu ni makundi ya mashirika yanayoratibu shughuli za kibinadamu kwa sekta mahususi (yaani, maji, afya, makazi, n.k.).

6 USAID/BHA hutumia neno Upangaji Salama wa Mipango badala ya Ujumuishaji wa Ulinzi, kwani istilahi ya Upangaji Salama wa Mipango inatambua uwezekano wa madhara ambayo misaada ya kibinadamu inaweza kusababisha au kuchangia na kuimarisha haja ya kuhakikisha kuwa misaada ya kibinadamu ni salama na inayolinda. Upangaji Salama wa Mipango hukuza jukumu la kuhakikisha usalama na kupunguza hatari za ulinzi kwa wafanyakazi wote, kwenye mipango yote.

Isitoshe, msaada wa kibinadamu unaweza kuzidisha mgogoro bila kukusudia au kusababisha mivutano mipya miongoni mwa wahusika wenyeji wakati rasilimali mpya zinapoonekana kuwa zinapendelea kikundi kimoja zaidi ya kingine. Nguvu hii inaweza kufanya walengwa wa msaada kuwa walengwa wa vurugu. Ili kukabiliana na hili, shirika la USAID litasaidia juhudi za kujumuisha makundi anuwai ya wahusika wenyeji katika kubuni na kutekeleza mpango, ikijumuisha na hasa makundi yaliyotengwa kihistoria, huku likiendeleza pia mabadiliko ambayo yanainua washirika mbalimbali wa eneo kwa majukumu ya uongozi ndani ya miundo ya uratibu wa msaada wa kibinadamu.

***MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU YA SEKTA:*** *MSAADA WA PESA TASLIMU NA VOCHA*

Matumizi ya pesa taslimu na msaada wa vocha yamekuwa yakiongezeka kwa kasi katika hatua zinazochukuliwa za kibinadamu tangu mwaka wa 2010, ikiwakilisha sehemu kubwa ya misaada ya kibinadamu ya shirika la USAID. Kwa mfano, kati ya miaka ya kifedha ya 2021-2023, shirika la USAID/BHA lilitenga kati ya dola bilioni 1.9 hadi dola bilioni 2.6 kama usaidizi wa pesa taslimu na wa vocha kwa mwaka, ikiwakilisha zaidi ya asilimia 20 ya bajeti ya kila mwaka ya shirika la USAID/BHA. Msaada wa pesa taslimu hupanua fursa za kusaidia ubora wa chaguo kwa watu binafsi na familia zilizoathiriwa na janga ili kutanguliza mahitaji yao muhimu, kama vile chakula, malazi, maji na mahitaji mengine, na hatimaye kutoa fursa ya uamuzi wa eneo husika katika hatua zinazochukuliwa za kibinadamu. Wakati masoko ya eneo yanapofanya kazi na bidhaa zinapatikana, pesa taslimu na vocha zinaweza kuwapa watu hawa manufaa huku zikisaidia kurejesha ukawaida kwa mifumo muhimu ya soko la eneo. Huku ikilenga kaya binafsi, mipango ya utumaju wa fedha inaweza kuwa na athari za mfumo mzima kwa kuongeza uwezo wa ununuzi wa wenyeji na kuchochea mahitaji kati ya biashara za eneo; ripoti ya ukaguzi ya Benki ya Dunia ya mwaka wa 2023 iligundua kuwa kwa kila dola 1 inayotumwa, uchumi wa eneo unaweza kukua kwa kiasi cha dola 2.

Uwasilishaji na uratibu wa utumiaji wa pesa taslimu kwa kiwango kikubwa unasimamiwa kupitia mpango mkubwa wa Umoja wa Mataifa (UN) au muungano unaoongozwa na shirika lisilo la kiserikali la kimataifa (INGO), ambao unaweza kuwezesha usimamizi bora wa ufadhili kulingana na kiwango cha kazi ya usimamizi ya wafanyakazi wa wahisani na katika baadhi ya mazingira inaweza kuruhusu utumiaji wa mbinu za ufaafu wa gharama, kama vile mazungumzo ya washirika kuhusu ada zinazofaa kwa huduma za kifedha na/au mpango. Juhudi zitabadilishwa na kuelekezwa katika utoaji wa fedha na usaidizi unaoongozwa na wenyeji na usaidizi kwa watekelezaji wa eneo zinaendelea katika ngazi za nchi na kimataifa, ingawa wanakabiliwa na changamoto sawa na juhudi za ujanibishaji katika sekta nyingine. Kwa sababu hizi, shirika la USAID/BHA limeshirikiana na Shirika la ushirikiano wa mafunzo pesa taslimu wa CALP (cash learning partnership CALP Network) ili kuwaita viongozi wakuu wa mashirika ya kutoa misaada ya kibinadamu ili kutetea na kuendeleza ahadi zetu za pamoja za kutoa misaada ya fedha na vocha inayozingatia watu na yenye ufanisi. Katika baadhi ya miktadha, shirika la USAID/BHA pia imegeukia wahusika wa eneo kama washirika wa moja kwa moja katika kutoa misaada ya pesa taslimu, kama vile kushirikiana na mashirika ya eneo kutoa msaada wa chakula kwa kutumia pesa taslimu nchini Kenya kukabiliana na ukame wa kihistoria wa mwaka wa 2023. Kati ya mwaka wa 2021-2023, washirika wa eneo RACIDA, Shirika la Msalaba Mwekundu la Kenya, na Shirika la Maendeleo la Wajir Kusini yalipeleka msaada wa muhimu katika kuokoa maisha nchini Kenya kwa usaidizi wa shirika la USAID/BHA wenye thamani ya zaidi ya dola milioni 17.7. Kwa kutekeleza kwa vitendo malengo matano yaliyoainishwa katika Sera ya LLHA, shirika la USAID linalenga kuafikia jukumu kubwa kwa mashirika ya eneo katika uratibu na utoaji wa zana muhimu ambazo hubadilisha nguvu na uwezo wa kubadilika kwa jamii zilizoathiriwa na janga.

## Washirika wa Kimataifa Wana Jukumu Muhimu katika Hatua za Kibinadamu

Sera ya LLHA inaangazia anuwai ya mifano ya ushirikiano na ushirikishwaji kati ya wahusika wa eneo na washirika wa utekelezaji wa kimataifa wa shirika la USAID, ambao mara nyingi hujulikana kama wapatanishi katika mfumo wa kutoa msaada wa kibinadamu.[7] Miundo hii hutanguliza kujifunza na kubadilishana maarifa na ujuzi, pamoja na uongozi wa wenyeji katika kipindi chote cha mpango wa kibinadamu. Mashirika ya INGO na mashirika ya kimataifa ya umma (PIOs) huwa kama njia kuu ambazo shirika la USAID hufadhili kazi ya mashirika ya kibinadamu ya eneo na huwa na jukumu muhimu la kushirikiana na kusaidiana na washirika wa eneo. Hata hivyo, mahusiano haya yanaweza kukumbana na changamoto. Washirika wa kimataifa wa utekelezaji wanaweza kushirikisha washirika wa eneo kwa kuchelewa katika mzunguko wa mpango wa kibinadamu ili kuhudumu hasa katika majukumu ya utekelezaji bila ushirikishwaji wa hapo awali katika kufanya maamuzi, kupanga mipango au kupanga mikakati, ambayo inaweza kuwa fursa iliyokoswa ya kuunganisha ujuzi na uwezo wa wenyeji. Vinginevyo, washirika wa utekelezaji wa kimataifa wanaweza kuendeleza umiliki wa wenyeji kwa kutoa kipaumbele kwa utaalamu wa wenyeji, uongozi wa wenyeji, mitandao ya watu wanaojuana na mali za watendaji wa ndani na kitaifa kupitia ushirikiano wa mapema na wa maana, muundo wa mpango shirikishi, uimarishaji wa uwezo unaolengwa, ushauri, na mbinu thabiti na za ubora wa ufadhili miongoni mwa aina nyingine muhimu za usaidizi. Mara nyingi, mashirika ya kimataifa yanaweza pia kuchukua jukumu muhimu katika kutoa ulinzi kwa kuwepo, kwa uwepo wao wa kimwili na utekelezaji wa itifaki za usalama na ulinzi kuzuia unyanyasaji au kushambuliwa kwa raia na wahalifu au watendaji wa vurugu. Mashirika ya INGO yanaweza pia kutumikia majukumu muhimu ya utetezi ili kuinua masuala muhimu kwa ajili ya hatua za kibinadamu zinazojikita kwenye kanuni kupitia majukwaa yao, ikiwezekana kwa hatari ndogo kuliko mashirika ya wenyeji.

### *KUWAJIBIKIA HATARI KWA PAMOJA*

Masharti mbalimbali ya USG—sheria, kanuni na sera—zinaendelea kuathiri kasi na upeo wa juhudi za ujanibishaji za shirika la USAID. Hatua hizi na vipengele vya tahadhari vimeundwa ili kuongeza uwazi na ufanisi wa utumiaji wa rasilimali za USG na kuzuia ulaghai, uharibifu na matumizi mabaya. Masharti changamano ya utiifu yanaweza kuleta changamoto kwa washirika wadogo au wa eneo wa utekelezaji, wengine ambao baadhi yao wana wafanyakazi wachache au hawana wafanyakazi wanaojitolea kabisa wa usimamizi wa hatari, udhibiti wa ndani na hatua nyingine za uzingatiaji ili kuchukua hatua ya masharti kuhusu hatari za usimamizi wa kifedha. Shirika la USAID linatathmini maeneo ambayo marekebisho ya utaratibu yanaweza kuongeza ufikiaji wa ufadhili huku yakiendelea kudumisha ulinzi unaohitajika. Isitoshe, mashirika ya INGO na NGO ya eneo husika huchukua hatari zingine, kama vile hatari za kiusalama, hatari za ulinzi, hatari za uaminifu, na hatari zinazohusishwa na sifa, wakati wa kutekeleza mipango ya shirika la USAID- na mipango mingine inayofadhiliwa na wahisani.[8] Sera ya LLHA inahimiza kupitishwa kwa mbinu ya kushiriki hatari, kulingana na [Mfumo wa Kuwajibikia Hatari kwa Pamoja wa mwaka wa 2023 wa Grand Bargain]. Mbinu ya kuwajibikia hatari kwa pamoja inahusisha ushirikiano kati ya wahusika wa kutoa msaada wa kibinadamu ili kutambua, kupunguza, na kudhibiti hatari, hivyo kuhakikisha kuwa hakuna mhusika yeyote anayekuwa na jukumu kubwa la hatari zinazohusiana na hatua zinazochukuliwa za kibinadamu.

7 Kulingana na Grand Bargain, wapatanishi wanafafanuliwa kama mashirika, mitandao, au taratibu (kama vile fedha zilizokusanywa) ambazo huleta upatanisho kati ya wafadhili na mashirika ya eneo husika kupitia utoaji wa ufadhili au usaidizi mwingine.


8 Chanzo: Utafiti wa Hatari kwa NGO yanazofadhiliwa na USAID, Matokeo ya Kibinadamu na Shughuli za Pamoja, 2019, https://www.humanitarianoutcomes.org/sites/default/files/publications/riskii_partnerships_global_study.pdf



Mradi wa Nawiri unaofadhiliwa na USAID/BHA laendeleza masuluhisho yaliyobuniwa katika eneo husika na endelevu kwa ajili ya utapiamlo unaoendelea katika ardhi kame na nusu kame ya Kenya. *Picha kwa hisani ya Mercy Corps.*

# KANUNI ZINAZOTOA MWONGOZO

Kanuni zifuatazo zinazotoa mwongozo hufafanua Sera hii na malengo yake. Baadhi ya kanuni hizi ni mahususi kwa sekta ya kutoa msaada wa kibinadamu, huku zingine zikiingiliana na juhudi pana za ujanibishaji za shirika la USAID.



- **Ubinadamu, Kutopendelea, Kutoegemea upande wowote na Uhuru:** Kama ilivyobainishwa hapo juu, kanuni hizi zinazotambulika kimataifa ndizo msingi wa hatua zote za kutoa msaada wa kibinadamu na zinatokana na sheria za kimataifa zinazoongoza utoaji wa misaada ya kibinadamu. Zinaongoza shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu za shirika la USAID pamoja na shughuli za washirika wetu wa kutoa msaada wa kibinadamu. Juhudi za kuendeleza shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu zinaoongozwa na wenyeji sharti zitiii kanuni hizi ili msaada ufikie watu wanaouhitaji zaidi, bila upendeleo au ubaguzi, huku zikizingatia viwango vya juu zaidi vya haki za binadamu, heshima na utu.

- **Ushirikiano wa Usawa na Ujumuishi:** Kanuni za usawa na ujumuishi, ambapo wahusika wote katika ushirikiano, ikijumuisha washirika wapya na wasio wa kawaida, pamoja na wawakilishi wa jumuiya zilizotengwa kihistoria, huchangia na kupokea manufaa kutoka kwayo, huzingatia vipengele vyote vya juhudi za ujanibishaji za shirika la USAID. Ushirikiano wa usawa na ujumuishi ni wa ushirikiano na wa uwazi, unaozingatia uwajibikaji wa pande zote, na unahitaji uwajibikaji kutoka kwa wadau wote. Zaidi ya hayo, Sera hii inawiana na kanuni zilizoainishwa katika Sera ya shirika la USAID ya Uimarishaji wa Uwezo wa Wenyeji, ambayo inaongoza mtazamo wa shirika la USAID wa kufikia matakwa ya sera kupitia uimarishaji wa uwezo.

- **Uwezo wa Kubadilika na Umaalumu wa Muktadha:** Vipimo, malengo, na mikakati ya hatua za kukabiliana na janga hufafanuliwa kulingana na muktadha, aina ya janga, mahitaji ya kibinadamu, eneo la kijiografia, mifumo ya uhamishaji wa watu, mazingira ya washirika, mienendo ya migogoro, masuala ya hatari na usalama na sifa za kitamaduni na lugha. Sera hii inalenga kuwa na uwezo wa kubadilika vya kutosha na inayoweza kuendana kulingana na uanuwai wa mazingira yanayobadilika na changamano, huku ikiwawezesha wahusika wa eneo na kukidhi mahitaji ya kipekee ya vikundi mbalimbali.

- **Kuzuia Madhara:** Shirika la USAID na hatua za washirika wa utekelezaji wa kimataifa zinaweza kuwaweka washirika wa eneo husika hatarini bila kukusudia au kuhamisha kiwango kisicho na uwiano cha hatari kwao, kuzidisha mivutano ya jaumuiya au kuwanyima haki baadhi ya watu. Kanuni ya Kuzuia Madhara inamaanisha shirika la USAID linalenga kuzuia na kupunguza athari mbaya zinazoweza kutokea kutokana na vitendo vyake kwa watu walioathirika. Sera hii inahimiza utumiaji wa kanuni ya Kuzuia Madhara katika ushirikiano wa kutoa misaada ya kibinadamu kati ya wenyeji na shirika la USAID.

### *KUSHIRIKI KATIKA MFUMO WA KUTOA MSAADA WA KIBINADAMU*

Shirika la USAID linatambua kuwa kuendeleza shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu zinaoongozwa na wenyeji huanza kwa kutambua kuwa si mazingira ya wahusika tu, lakini pia mahusiano kati ya wahusika—wa eneo, kitaifa na kimataifa—huamua kiwango cha hatua zinazoongozwa na wenyeji. Mfumo wa kutoa msaada wa kibinadamu unajumuisha mashirika mbalimbali, mashirika, na mitandao inayowezesha utoaji wa msaada wa kibinadamu. Mtazamo wa shirika la USAID kwa shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu zinazoongozwa na wenyeji utatumia fursa zaidi ya ushirikiano wake wa moja kwa moja na uhusiano wa ufadhili ili kutetea uongozi wa wenyeji katika ngazi ya kitaifa na kimataifa, huku ikitarajia na kuzuia matokeo yasiyotarajiwa pia.

# UPEO WA SERA

Sera ya LLHA ni sehemu moja ya mbinu ya jumla ya ujanibishaji ya Shirika, inayolenga kutoa msaada wa kibinadamu katika mwendelezo unaojumuisha hatua zinazochukuliwa wakati wa hali ya dharura, urejeshaji wa shughuli za kawaida haraka, ustahimilivu na shughuli za DRR.



Wakaazi na mashirika ya eneo husika yaliweza kufikia maeneo yaliyoathiriwa katika mkoa wa kaskazini-magharibi wa Idlib nchini Syria kufuatia tetemeko la ardhi la 2023, wakiwatafuta wahasiriwa katika majengo yaliyoporomoka na kutathmini hali ya barabara. *Picha ilipigwa na Omar Haj Kadour/AFP.*

## Dharura Zinazotokea kwa Haraka

Katika hali za dharura zinazotokea kwa haraka, uhusiano na ujuzi wa jamii za wenyeji, ukaribu na maeneo yaliyoathirika na ufikiaji wa haraka wa bidhaa ni muhimu ili kukidhi mahitaji muhimu haraka. Mashirika ya eneo husika mara nyingi yana nafasi nzuri zaidi ya kuangazia hali hizi halisi na kushughulikia masuala haya, ingawa yanaweza kuathiriwa moja kwa moja na majanga. Kwa sababu hizi, ushirikiano wa kuoanisha wahusika wa eneo na mashirika makubwa ya kimataifa yenye ufikiaji ulio tayari wa bidhaa, uwezo usafirishaji wa bidhaa na rasilimali za kiufundi unaweza kuwa na ufanisi hasa. Hata hivyo, matukio ya hatua za haraka zinazochukuliwa yanaweza kutofaa kwa juhudi za shirika la USAID za kutambua na kuendeleza ushirikiano mpya wa kibinadamu na wenyeji, kwani kuendeleza ushirikiano huu huchukua muda na rasilimali kwa pande zote mbili. Shirika la USAID linapanua uwekezaji katika ramani ya mazingira ya washirika wanaotoa msaada wa kibinadamu kwa kuzingatia mashirika ya eneo na yasiyo ya kawaida, huku ikianzisha mbinu za utoaji wa haraka wa ufadhili—kabla ya janga kutokea—hiyo inaweza kusaidia kuwezesha uchukuaji wa hatua inayoongozwa na wenyeji wakati wa janga.[9] Msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji katika hali za dharura zinazotokea kwa haraka—ikijumuisha shughuli ambazo zinaimarishwa na washirika wa kimataifa—unaweza kuwa wa haraka zaidi, wenye utambuzi zaidi kwenye miktadha mahususi ya eneoi na kuchukua hatua zaidi kulingana na mahitaji ya jamii kuliko yale yanayowatenga washirika wa eneo husika.



Mshirika wa ndani wa USAID/BHA liitwalo ABCom lawafikia wakimbizi wa ndani katika jimbo la Kivu Kaskazini katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na usaidizi wa kushughulikia mahitaji yao ya dharura ya chakula na mahitaji mengine ya kimsingi. *Picha kwa hisani ya ABCom.*

## Migogoro ya Muda Mrefu na Hali Zingine Changamano za Dharuras

Wakati wa migogoro ya muda mrefu na hali zingine changamano za dharura, shughuli za wahusika wa kutoa msaada wa kibinadamu wa eneo na wa kimataifa mara nyingi hutatizwa na vikwazo vya ufikiaji na hatari za usalama na ulinzi. Hatari hizi huchangiwa na hatari za usimamizi wa fedha, kisheria na sifa, pamoja na vikwazo vinavyoweza kutolewa na serikali-mwenyeji vinavyolenga mashirika na wafanyakazi wa kimataifa. Ingawa mashirika ya eneo husika yanakumbana na vikwazo sawa, uwepo wao endelevu, mitandao ya jamii, uhusiano na nguvu za eneo husika na uelewa wa mienendo ya migogoro mara nyingi hurahisisha ufikiaji wa maeneo yaliyoathirika na utoaji wa msaada wa kibinadamu. Hata hivyo, ufikiaji na ukaribu wa wahusikai wa eneo husika kwa maeneo yaliyoathirika ambayo mara nyingi si salama yanaweza pia kusababisha hatari za usalama

9 Mbinu ya USAID ya kutambua watendaji wa ndani kupitia uchanganuzi wa mazingira ya washirika imeainishwa na Mpango Mpya wa Ushirikiano wa USAID..

na ulinzi kwa washirika wa eneo na wafanyakazi wa ndani wa mashirika ya kimataifa. Zaidi ya haya, utoaji wa msaada wa kibinadamu kwa ufafanuzi huingiza rasilimali muhimu na umakini wa kimataifa katika mapambano ya nguvu za maeneo yenye ukosefu wa utulivu, ambayo yanaweza kubadilisha mwelekeo na mienendo ya mgogoro kwa kuwawezesha baadhi ya watendaji na kuwanyima uwezo wengine. Kwa kuzingatia matokeo haya, sheria ya shirika la USAID kuhusu utoaji wa msaada wa kibinadamu moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kupitia washirika wa eneo katika mazingira ya migogoro sharti usaidiwe na kanuni za kibinadamu zinazotambulika kimataifa za, wajibu wa kutunza, Kuzuia Madhara na kanuni zinazozingatia migogoro, pamoja na uchanganuzi mzuri wa migogoro na uchumi wa kisiasa. Msaada unapaswa pia kutolewa na kuwa na uwezo wa kubadilika unaohitajika ili kukabiliana na hali zinazobadilika inapohitajika. Ikiwa shirika la USAID, pamoja na washirika wake, yatazuia hatari hizi kwa ufanisi, dharura za muda mrefu zinaweza pia kutumika kama nafasi za uwekezaji wa muda mrefu katika ushirikiano na wenyeji, ujenzi wa mtandao na wenyeji, uimarishaji wa uwezo unaolengwa, utetezi wa kuunga mkono uongozi wa wenyeji na kuimarisha uthabiti na mienendo ya amani.

## Urejeshaji wa Hali ya Kawaida Haraka, Kupunguza Hatari, na Ustahimilivu (ER4)

Urejeshaji wa Hali ya Kawaida Haraka, DRR, na baadhi ya mipango ya ustahimilivu hutoa fursa zaidi za kuongeza ushirikiano uliopo na mpya na wenyeji. Kwa shinikizo ndogo la kuchukua hatua ya moja kwa moja kwa moja kwenye eneo husika, shirika la USAID na washirika wa ene husika wana fursa ya kushiriki majadiliano ya makusudi kuhusu kujenga ushirikiano wa kimkakati, wa muda mrefu, pamoja na kupitisha utengenezaji wa pamoja na "Miundo Bora na Utekelezaji".[10] Maarifa ya hatari ya eneo husika na mahusiano mbalimbali ya jumuiya ni muhimu sana katika kubuni, kuongoza, na kutekeleza masuluhisho. Isitoshe, DRR yenye ufanisi na ubunifu na mipango ya ustahimilivu hunufaika kutokana na uwekezaji wa miaka mingi ambao unategemea uwepo endelevu na kujitolea kwa muda mrefu ambako washirika wa eneo wanaweza kutoa. Uwekezaji huu wa ER4 unaweza kuwezesha washirika wa eneo husika kuongoza na kuchukua hatua yenye ubora wa juu bila usaidizi wa kimataifa kuhitajik.



Kwa usaidizi wa USAID/BHA, vijana nchini Dominika wajitayarisha kuongoza shughuli za kukabiliana na maafa katika jumuiya zao kama sehemu ya Kamati za Hatua za Dharura za Vijana (YEAC), ikijumuisha kwa kushiriki katika mazoezi ya kuiga shughuli za kukabiliana na dharura. *Picha kwa hisani ya YEAC Dominika.*

**ER4**
- Long-term partnerships
- Co-creation/Refine and Implement processes
- Multi-year Investments
- Creative funding models
- Capacity strengthening

**Rapid Response**
- Intermediary rapid support systems
- Leverage existing partnerships
- Partner pivots
- Simplified funding requirements
- Rapid Response Funds

**Protracted Crises**
- Local network access
- Systems-strengthen approaches
- Community-based program design, budgeting, evaluations
- Local engagement in humanitarian coordination structures

**Equitable local partnership that meet humanitarian needs in a given context**

10 Kuboresha na Kutekeleza ni mbinu ya shughuli za usalama wa chakula zenye mwelekeo wa ustahimilivu zinazoungwa mkono na USAID/BHA. Mbinu hiyo hutumia kipindi cha uboreshaji kabla ya utekelezaji kamili wa ufadhili, ambapo washirika wanaotekeleza huboresha muundo wa shughuli kulingana na ushahidi na maoni ya wadau, kuwekeza katika ukuzaji wa wafanyakazi, na kuweka mikakati ya utekelezaji kulingana na kanuni na muktadha wa eneo husika.

## Miunganisho ya HDP (HDP Nexus)

Ingawa Sera ya LLHA itatumika kwa mazingira mengi ya shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu, utekelezaji utatofautiana kulingana na miktadha ya kikanda na ya nchi husika, haswa kote kwenye Miunganisho ya HDP (HDP Nexus). Uwiano wa HDP unalenga kuongeza athari na uendelevu wa mipango kwa kukuza mawasiliano, uratibu na inapowezekana, ushirikiano katika wigo wa utoaji wa misaada ya kibinadamu, maendeleo na amani ili kujenga aina ya hali salama, ya amani ambayo inapunguza haja ya utoaji wa msaada wa kibinadamu kwa muda mrefu. Kwa hivyo, wahusika wa eneo waliounganishwa kwenye mitandao ya rasilimali, walio tayari kutazamia na kukabiliana na majanga na wanaodhihirisha ustahimilivu katika kukabiliana na changamoto tata ni muhimu kwa mbinu ya Miunganisho ya HDP (HDP Nexus). Hatimaye, Sera hii inalenga kutambua shirika la wahusika wenyeji na jumuiya zilizoathiriwa na janga ili kufafanua na kusisitiza majukumu yao katika kuhakikisha hatua itakayochukuliwa ya kukabiliana na janga la kibinadamu.

## Ushirikishi wa Wenyeji ni Mchakato

Kwa kutambua hali ya ujanibishaji inayokua na inayotokana na muktadha, shirika la USAID linarejelea Wigo wa Maendeleo Yanayoongozwa na Wenyeji kuelezea aina mbalimbali za mbinu ambazo Shirika, washirika wake na jumuiya zinaweza kushirikiana kwa pamoja ili kuhamishia mamlaka ya kuweka ajenda na kufanya maamuzi mikononi mwa wahusika ambao ni wenyeji.[11] Ili kutekeleza kwa kikamilifu Sera ya LLHA, kuna uwezekano kuwa shirika la USAID litabadili ushirikiano katika miktadha ya kibinadamu kuelekea haki ya wigo, kuhakikisha kuwa ushirikiano na wahusika ambao ni wenyeji unazidi ya ushiriki wa taarifa na mashauriano na kuelekea kwa ugawaji mkubwa wa mamlaka na hatimaye uongozi wa wenyeji, kama ilivyoonyeshwa kwenye mchoro wa hapo juu. Mabadiliko haya yanaweza kujumuisha ufadhili wa moja kwa moja zaidi pamoja na miundo ya ushirikiano iliyoimarishwa.




### *UTOAJI WA MSAADA WA KIBINADAMU UNAOONGOZWA NA WENYEJI NA TABIANCHI*

Kote duniani, hatari zinazohusiana na tabianchi huathiri kwa kiwango kikubwa jamii maskini zaidi na zilizotengwa kihistoria. Watu wanaoishi katika maeneo haya mara nyingi wako katika nafasi nzuri zaidi ya kubuni na kuelekeza hatua za uingiliaji kati zinazofaa zaidi kukidhi mahitaji yao. Shirika la USAID linajitahidi kusaidia jumuiya kujiandaa na kuzoea athari za hatari zinazotokana na tabianchi kupitia masuluhisho yanayoongozwa na wenyeji katika kupunguza hatari kutokana na janga, ikiwa ni pamoja na onyo la mapema, utayari na shughuli za kukabiliana nazo. Juhudi za shirika la USAID zinaonyesha uidhinishaji wa Mkataba wa Serikali Kuu ya Marekani (USG) wa Mkataba wa Tabianchi na Mazingira kwa Mashirika yanayotoa Msaada wa Kibinadamu, unaojumuisha kukumbatia uongozi wa wahusika na jumuiya za wenyeji kama mojawapo ya ahadi saba za Mkataba.

11 Wigo wa Maendeleo Yanayoongozwa na Wenyeji ni zana iliyotengenezwa na Mpango wa USAID wa Maendeleo Yanayoongozwa na Wenyeji ili kusaidia USAID na washirika kufikiria kuhusu umuhimu wa maendeleo yanayoongozwa na wenyeji kwa vitendo. USAID lilitoa wigo kutoka Oxfam America na Mfumo wa Tathmini ya Ushirikiano wa Wenyeji wa Save the Children.

***UMUHIMU WA KUFAHAMU MASUALA NYETI KUHUSIANA NA MIGOGORO***

Msaada wote wa kigeni hubadilisha hali na uwiano wa nguvu katika mgogoro. Shirika la USAID hupunguza hatari hizi kwa kuchanganua mienendo ya migogoro na uhusiano kati ya wahusika ambao ni wenyeji na jinsi utoaji wa msaada wa kibinadamu unavyoingiliana na kuathiri wakazi, ikiwa ni pamoja na makundi yaliyo na uwakilishi mdogo na yaliyotengwa kihistoria. Shirika la USAID hutumia maarifa haya katika awamu zote za kuchukua hatua ili kutoa msaada unaoepuka kuzidisha mienendo ya migogoro na kuchukua kila fursa kuimarisha mwingiliano mzuri, ustahimilivu unaokuza mazingira salama zaidi.

# UTUMIAJI WA SERA

## Maono ya Sera

*Shirika la USAID linaweka jumuiya za wenyeji kama msingi wa kazi ya kibinadamu na kutoa usaidizi kwa mfumo wa kibinadamu unaofanya kazi kwa misingi ya maamuzi na vipaumbele vya wenyeji, unaoakisi mahitaji na mapendeleo ya vikundi vilivyoathirika. Mafanikio katika juhudi za shirika la USAID za kuendeleza utoaji wa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji hayafafanuliwi na shabaha moja ya ufadhili, uzinduzi wa michakato mipya au idadi mahususi ya washirika wa eneo husika. Badala yake, mafanikio yanapatikana wakati mbinu za shirika la USAID za kufanya kazi kwa maana zinashirikisha washirika wa ndani ili kuongoza mipango na hatua za kibinadamu zenye ufanisi.*



## ONGEZA KIASI NA UPATIKANAJI WA UFADHILI KWA MASHIRIKA YA KUTOA MISAADA YA KIBINADAMU YA ENEO HUSIKA

*Kupunguza vizuizi vya ufadhili kwa wahusika wanaotoka eneo husika kunaafikiwa kwa sehemu kwa kutumia mitindo ya ushirikiano inayoweza kubadilika ili kukidhi mahitaji anuwai ya washirika wa kibinadamu katika miktadha inayobadilika ya hatua zinazochuliwa.*

Shirika la USAID hutumia ufadhili kusaidia jumuiya ya watu wanaotoa msaada wa kibinadamu ili kukidhi mahitaji muhimu duniani kote. Shirika la USAID linaamini kwa dhati kuwa maamuzi bora zaidi ya ufadhili yanahitaji nia, mitandao rasmi ya watu wa uwajibikaji, kipimo cha hatari na rasilimali za kutosha za kifedha na wafanyakazi. Shirika la USAID limejitolea kuelekeza asilimia 25 ya ufadhili moja kwa moja kwa wahusika wa eneo hilo ifikapo mwaka 2025 na kuhakikisha kuwa asilimia 50 ya shughuli zetu zinaongozwa na wenyeji ifikapo mwaka wa 2030. Wakati huo huo, mashirika ya eneo husika mara kwa mara yanataja vikwazo mbalimbali vya ushirikiano wa moja kwa moja, ikiwa ni pamoja na mwongozo changamano wa maombi, lugha ya Kiingereza na masharti ya kabla ya kupewa ufadhili, matarajio ya kuripoti, urejeshaji wa gharama usiotosha, ukosefu wa ufikiaji kwa wafanyakazi wa shirika la USAID, kipindi cha muda mfupi wa mradi usio endelevu na mafunzo duni au usaidizi wa kusawazisha mahitaji ya wafadhili na mahitaji ya uundaji wa mpango.

Katika utafutaji wa ushirikiano mpya wa kibinadamu na wenyeji, shirika la USAID litatumia mtazamo pana zaidi kwa miundo ya ushirikiano iliyopo na kupanua mbinu bora za uundaji wa ufadhili mahiri na unaoweza kubadilika. Hii ni pamoja na kutumia mbinu shirikishi na za kiubunifu kwa muundo wa hatua zinazochukuliwa, tathmini na ujifunzaji unaoendeshwa na ufafanuzi wa eneo husika wa mafanikio ya mpango na kuongeza fursa za kuimarisha uwezo na kubadilika ili kugeuza na kuweka vipaumbele kadiri mahitaji ya utoaji wa misaada ya kibinadamu yanavyobadilika. Kando na juhudi zinazoendelea za shirika la USAID za kupunguza vizuizi vya kujiunga na mashirika ya eneo husika, shirika la USAID linakagua tena mzunguko wake wa mpango wa utoaji wa msaada wa kibinadamu kwa lengo la kupanua wigo wa washirika wake na kuwezesha kuchukua hatua za haraka na za ufanisi za kibinadamu. Juhudi hizi zitafahamisha hatua za kurahisisha michakato ya utoaji wa ufadhili wa kibinadamu, kama vile mwongozo wa maombi uliorahisishwa na kufanya mawasiliano na mafunzo kuhusu michakato hii ili shirika la USAID liwe kiongozi na mshirika mzuri zaidi wa kibinadamu, ikiwa ni pamoja na kwa wahusika wa eneo husika.

### HATUA MUHIMU:

- **Kujenga ushirikiano wa kibinadamu na mashirika ya eneo husika, ikiwa ni pamoja na kupitia ufadhili wa moja kwa moja,** unaofafanuliwa na ramani ya mazingira ya washirika, ufikiaji wa mapema na uliopanuliwa kwa wahusika mbalimbali wa eneo wanaochukua hatua za kibinadamu na kuzingatia rasilimali zinazohitajika ili kupunguza na kudhibiti hatari.

- **Kutumia rasilimali za shirika la USAID na USG, mahusiano, utaalamu, na diplomasia ya kibinadamu ili kuhimiza washirika wa kibinadamu wa mashirika ya PIO na INGO kuunda mahusiano zaidi yenye usawa, ujumuishi, na uendelevu na mashirika ya wenyeji,** ambayo yanajumuisha ubadilishanaji wa uwezo na ujuzi na kujumuisha ufidiaji wa gharama kamili kwa waliopewa ufadhili mdogo.

## KUIMARISHA UWEZO WA SHIRIKA LA USAID WA KUJENGA USHIRIKIANO WA KIBINADAMU

*Kuongeza kwa ushirikiano wa kibinadamu wa hali ya juu kutahitaji tathmini zaidi ya rasilimali watu na za uendeshaji za shirika la USAID.*

Kuendeleza utoaji wa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji kunahitaji nia na umiliki kote katika Shirika. Kuongeza idadi na ubora wa ushirikiano wa eneo, kuchakata idadi kubwa zaidi ya ufadhili wa moja kwa moja kwa washirika wapya, kuwekeza katika mbinu za kuimarisha uwezo zinazofaa kwa miktadha ya kibinadamu inayobadilika na kutetea michakato na miundo ambayo inatanguliza watendaji wa ndani na jamii inahitaji uwekezaji mkubwa wa wakati na. rasilimali watu na uendeshaji. Kama sehemu ya juhudi pana za ujanibishaji za Shirika, shirika la USAID linakuza shughuli za maendeleo na utoaji wa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji kupitia mwongozo maalum, mafunzo, na rasilimali. Hii itawapa wafanyakazi taarifa na ujuzi unaohitajika ili kutekeleza malengo ya ujanibishaji katika hatua zote za utengenezaji wa ufadhili na usimamizi wa mpango, pamoja na kuunganisha kanuni muhimu na ujumbe wa utetezi katika sera na juhudi za kimataifa za utetezi wa umma. Mwongozo wa kiufundi na ujumbe thabiti wa malengo muhimu ya ujanibishaji na hatua za kipaumbele katika sekta zote, maeneo ya kijiografia na miktadha ya hatua zinazochukuliwa itasaidia uwiano mkubwa wa juhudi za ujanibishaji na kusaidia ufahamu ulioongezeka wa zana za vitendo na mbinu za kuendeleza ushirikiano na wenyeji. Shirika la USAID pia litatathmini haja ya wafanyakazi wa ziada kusaidia hatua za utoaji wa msaada wa kibinadamu zinazoongozwa na wenyeji.

Ukaguzi wa shirika la USAID wa mzunguko wake wa upangaji wa mpango wa kutoa msaada wa kibinadamu utatoa uundaji upya wa michakato na mifumo yake ya upangaji wa kimkakati, utoaji wa ufadhili, ufuatiliaji wa mpango, tathmini na mafunzo. Usanifu upya utawezesha shirika la USAID kuwa mshirika bora wa kibinadamu, ikiwa ni pamoja na wahusika wa eneo husika, kuanzia na mchakato wa mipango wa ndani wa wasifu ambao unajumuisha masuala ya ujanibishaji mapema katika mipango ya kimkakati. Kukuza ujuzi na ustadi wa wafanyakazi wa utoaji wa misaada ya kibinadamu wa shirika la USAID kwenye michakato iliyosanifiwa upya, iliyoratibiwa na iliyorahisishwa ya kutoa ufadhili itakuwa muhimu kwa uwezo wetu wa kujenga ushirikiano wa kibinadamu na wenyeji. Ili kutekeleza mabadiliko haya, shirika la USAID litatathmini marekebisho yoyote ambayo yanaweza kuhitajika kwa uwezo wa sasa, wafanyakazi na miundombinu.

### HATUA MUHIMU:

- **Kuwawezeshe wafanyakazi wa shirika la USAID kuwa watetezi wa shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji** kwa kusaidia utoaji wa ujumbe madhubuti, utumishi wa kujitolea na nyenzo muhimu za kiufundi katika ofisi, mipango na mikondo ya kazi.

- **Kutanguliza usimamizi wa maarifa ili kukuza ujifunzaji kutoka kwa mbinu za uchukuaji wa hatua za kibinadamu zinazoongozwa na wenyeji,** ikiwa ni pamoja na kupata masomo muhimu yaliyopatikana katika sekta zote, maeneo ya kijiografia, na miundo ya ushirikiano na urekebishaji wa utaratibu na marudio yaliyojikita katika msingi wa ushahidi unaokua wa shughuli za utoaji wa msaada wa kibinadamu zinazoongozwa na wenyeji.

## KUONGEZA UIMARISHAJI NA USHIRIKIANO WA UWEZO, PAMOJA NA KUJIFUNZA KWA PAMOJA KATIKA USHIRIKIANO WA SHUGHULI ZA KIBINADAMU

*Shughuli za kuimarisha uwezo wa utoaji wa misaada ya kibinadamu na ushiriki hujitahidi kuelewa uwezo uliopo wa jumuiya, kutambua fursa za kuwekeza katika uboreshaji wa mfumo na kuendeleza michakato ya kujumuisha ushiriki wa kujitolea wa uwezo katika utoaji wa msaada wa kibinadamu.*

Kuimarisha uwezo wa wenyeji wa kukabiliana na mishtuko ni sehemu ya msingi ya mbinu ya shirika la USAID kwa suala la utoaji wa msaada wa kibinadamu, ambapo jumuiya zilizoathiriwa zaidi na migogoro zina jukumu kubwa katika kufafanua vipaumbele vya utayari, uchukuaji wa hatua, unafuu, ahueni na kujenga ustahimilivu. Wakati huo huo, shughuli za kuimarisha uwezo zinazolenga wahusika wanaotoa msaada wa kibinadamu kwa sasa zinatofautiana sana katika mbinu zao, rasilimali, na athari; katika baadhi ya matukio, mbinu za kuimarisha uwezo zinaweza kuimarisha usawa uliopo wa nguvu, hasa wakati uwezo muhimu unapofafanuliwa na mashirika ya wahisani pekee. Juhudi zaidi za ushirikiano zinahitajika ili kusaidia mashirika yote ya eneo husika ili kufafanua na kufikia malengo yao.

Sera hii inaunga mkono upatanishi wa juhudi za uimarishaji wa uwezo wa kibinadamu na kanuni muhimu za uwezo zilizoainishwa katika Sera ya Uimarishaji wa Uwezo wa Wenyeji ya shirika la USAID, ikijumuisha mabadiliko mapana kuelekea mbinu inayotegemea mali ya kuimarisha uwezo, kwa kuzingatia utambuzi kuwa washirika wote wana uwezo mkubwa uliopo. Hizi kwa kawaida hujumuisha ujuzi wa kina wa mifumo ya eneo husika; taarifa ya wakati halisi kuhusu mahitaji ya usambazaji na vifaa; uwezo wa kufafanua na kutathmini mahitaji ya kibinadamu kati ya wenyeji; ufikiaji wa watu ambao ni vigumu kuwafikia; ufahamu wa mienendo ya kihistoria, kisiasa na migogoro; na utaalam wa kiufundi unaofaa kwa muktadha wa eneo hilo. Mara kwa mara, wafadhili na mashirika ya kimataifa hukosa uwezo huu muhimu na wanaweza kushindwa kuzitambua kama hivyo. Kwa sababu hii, katika kutafuta njia za usawa zaidi za ushirikiano na hatua zinazochukuliwa za kibinadamu zinaozoongozwa na wenyeji, Sera hii inakuza mbinu inayotegemea mali inayoegemezwa katika kubadilishana uwezo, mchakato wa kuimarisha ufanisi wa mtu binafsi na mfumo kupitia uwekezaji katika kubadilishana maarifa na kujenga ujuzi ambao unatanguliza kipaumbele cha mafunzo ya pamoja na usawa kati ya watendaji, kulingana na utambuzi wa uwezo uliopo.

### HATUA MUHIMU:

- **Kuwekeza katika miundo bunifu ya kuimarisha uwezo na -kukushiriki mitindo ya ushirikiano wa kibinadamu,** hasa upangaji wa mipango inayozingatia uwezo unaounga mkono utaalamu wa wenyeji, uwezo uliopo wa jumuiya, na mafunzo ya pamoja.

- **Kuweka maarifa ya wenyeji katika vipengele vyote vya hatua zinazochukuliwa katika utoaji wa msaada wa kibinadamu,** kupitia usaidizi wa kujitolea wa watafiti wa Nchi Zinazokua na Nchi zenye Maendeleo Duni, taasisi za utafiti na wataalamu wa masuala katika kubuni, utekelezaji na tathmini ya mpango.

## KUTETEA WA UONGOZI WA WENYEJI KATIKA SHUGHULI ZA KIBINADAMU

*Uongozi wa wenyeji ni sehemu muhimu ya utoaji wa msaada wa kibinadamu wenye ufanisi na uendelevu na unahitaji wahusika wa eneo, kitaifa na kimataifa kutambua aina mbalimbali za ujuzi na uzoefu ambao huwapa wahusika wa eneo husika uwezo wa kutekeleza majukumu ya kufanya maamuzi.*

Kulingana na kanuni inayoongoza ya ushirikiano wenye usawa na jumuishi, shirika la USAID linalenga kuuunga mkono mbinu za utoaji wa msaada wa kibinadamu ambazo zinaweka utofauti wa wahusika wa eneo na jumuiya kama msingi katika maamuzi na muundo wa mpango, huku ikitetea pia mabadiliko ambayo yanainua washirika mbalimbali wa eneo kwenye majukumu ya uongozi ndani ya mifumo ya uratibu iliyo nchini inayoongozwa na wanchi wa nchi husika. Shirika la USAID limejitolea kuhakikisha kuwa asilimia 50 ya shughuli zetu zinaongozwa na wenyeji ifikapo mwaka wa 2030, kama inavyofafanuliwa na Kiashirio cha Mipango Inayoongozwa na Wenyeji. Uongozi wa wenyeji unajumuisha uwezo wa wahusika wa eneo husika kuweka ajenda zao wenyewe, kubuni masuluhisho na kutumia uwezo wao, uongozi, na rasilimali ili kufanikisha masuluhisho hayo. Katika kutetea uongozi wa wahusika wa eneo hilo, shirika la USAID linasisitiza juu ya umuhimu wa kuwawezesha wawakilishi wa makundi mbalimbali ya kijamii, badala ya kuwapandisha cheo tu wale ambao tayari wako kwenye nafasi za madaraka katika ngazi ya kieneo.

Kipengele muhimu cha umiliki na uongozi wa wenyeji ni uwezo wa wahusika wa eneo husika kufafanua na kushawishi mikakati ya utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa eneo lililoathiriwa katika miktadha mingi ya uendeshaji, ambayo inategemea vipaumbele vinavyotambuliwa na uanuwai wa wanachama katika jumuiya za eneo husika. Shirika la USAID linatafuta fursa za kuwaweka wahusika mbalimbali wa eneo hilo kwa utaratibu zaidi, ikiwa ni pamoja na wale ambao wametengwa kihistoria, katika michakato ya kupanga na kufanya maamuzi, ikiwa ni pamoja na kupitia uundaji wa pamoja, majukwaa ya Uwajibikaji kwa Watu Walioathiriwa (AAP) na usaidizi wa moja kwa moja kwa ajili ya utoaji wa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji. Kwa kuzingatia kujitolea kwa Shirika AAP, Shirika la USAID linatumia michakato shirikishi inayojumuisha maoni ya wenyeji katika kuunda mikakati na mipango ya muktadha mahususi.

### HATUA MUHIMU:

- **Kuendeleza mazoea mazuri kwa uongozi wa weneji katika nyanja zote za utoaji wa msaada wa kibinadamu;** hii ni pamoja na ushirikishwaji kamili wa mashirika mbalimbali ya eneo hilo katika Ukaguzi mahususi wa Mahitaji ya Kibinadamu na Mipango ya Hatua zinazochukuliwa za Kibinadamu, pamoja na majukumu mashuhuri ya ushauri na ufanyaji wa maamuzi wa wahusika wa eneo hilo ndani ya HCT, vikundi, na majukwaa ya vikundi, ambayo yote huchangia katika upangaji wa hatua inayochukuliwa, kuweka vipaumbele, uratibu, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini.[12]

- **Kuimarisha uundaji wa pamoja wa mipango ya utoaji wa misaada ya kibinadamu katika uundaji wa mpango, kupanua mbinu za kuwajibikia hatari kwa pamoja, kubuni mbinu za kusaidia uwajibikaji wa pande zote na viwango vya mafunzo na kujitolea kutumia njia za mawasiliano za moja kwa moja na za uwazi,** zote ambazo mashirika ya eneo hilo yanatambua mara kwa mara kuwa hazipo lakini zinahitajika kabisa katika mifumo ya utoaji wa misaada ya sasa ya kibinadamu.

12 Muhtasari wa mahitaji ya kibinadamu (HNO) unatolewa ili kusaidia HCT katika kuelewa athari na mabadiliko ya janga na kutoa mwongozo kwa mipango ya kukabiliana nalo; Mpango wa Kutoa Usaidizi wa Kibinadamu (HRP) unaeleza maono ya pamoja ya jinsi ya kukabiliana na mahitaji yaliyotathminiwa na yaliyoelezwa ya watu walioathirika.

## KUTUMIA DIPLOMASIA YA KIBINADAMU NA UONGOZI WA SERA

*Ingawa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji unahitaji ushirikishwaji wa ngazi ya kitaifa na jumuiya, hatua ya kimataifa inahitajika ili kubadilisha mfumo wa kimataifa wa kutoa msaada wa kibinadamu kwa njia zinazounda nafasi ya ushiriki wa wenyeji na uongozi wa kweli mashinani.*

Kama mhisani mkubwa zaidi duniani wa kutoa misaada ya kibinadamu, shirika la USAID lina fursa—na wajibu—kuhudumu kama mtetezi wa kimataifa na kiongozi mwenye utaalamu, kwa kutumia uwezo wetu wa kiutawala, ushirikiano, sauti na zana nyinginezo za diplomasia ya kibinadamu ili kuchochea mabadiliko makubwa zaidi kuelekea kwa shughuli za kutoa misaada ya kibinadamu inayoongozwa na wenyeji.

Hatua inayochukuliwa ya sera ya kiwango cha kimataifa ili kuendeleza shughuli za maendeleo na kutoa misaada ya kibinadamu inayoongozwa na wenyeji ni muhimu kama vile hatua ya ngazi ya kieneo ili kubadilisha utamaduni, tabia na mifumo ili kuunda nafasi ya ushiriki na uongozi halisi wa wenyeji.

Shirika la USAID litaendelea kutumia ushirikiano baina ya nchi na majukwaa ya kimataifa ili kutetea na kuoanisha mbinu zenye mwelekeo wa matokeo za wafadhili na washirika wanaotekeleza kwa pamoja ili kuziba pengo kati ya sera na mbinu za kutoa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji. Mara kwa mara, Shirika hutafuta maoni kutoka kwa washirika wa eneo na wahusika wengine wa kitaifa ili kuhakikisha kuwa sauti za ndani zinaarifu moja kwa moja utoaji wa ujumbe wa utetezi wa kimataifa. Isitoshe, Shirika litaendelea kutafuta fursa za kutumia zaidi mifumo ya ufadhili wa misaada ya kibinadamu ya wafadhili mbalimbali, ikiwa ni pamoja na fedha zilizotengwa kwa ajii ya kutoa msaada wa kibinadamu na mbinu zingine za kibunifu za kuelekeza rasilimali zaidi kwa wahusika wa eneo husika na kitaifa.

### HATUA MUHIMU:

- **Kushirikiana na jumuiya ya wahisani wa kufadhili shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu kwa pamoja ili kupunguza vikwazo kwa ushirikiano na wenyeji** kwa kutumia mifumo ya pamoja na mifumo ya udhibiti wa hatari ili kurahisisha uangalizi unaostahili, kuripoti kwa washirika na michakato mingine.

- **Kutetea miundo ya ushirikiano na wenyeji yenye usawa na jumuishi miongoni mwa uongozi wa Mashirika ya INGO na PIO na katika majukwaa ya ngazi ya juu ya kibinadamu,** kwa kuzingatia mafunzo kutoka kwa wasifu wa kutoa misaada ya kibinadamu ya Shirika, miongoni mwao ikiwa ni pamoja na uundaji wa pamoja wa mpango, msaada wa kiufundi na msaada wa kuimarisha uwezo kwa wahusika wenyeji na mashirika ya kitaifa ya kudhibiti majanga, huku pia yakitafuta fursa kubwa zaidi ya kuwezesha mashirika ya eneo na vikundi vya jamii kuongoza uhakiki wa utayari wa kukabiliana na majanga na hatua ya kuchukua wakati wa hali ya dharura.

- **Kutumia mamlaka ya kuwaleta mashirika pamoja katika mijadala ya kibinadamu ili kusaidia juhudi za kutoa msaada wa kibinadamu zinazoongozwa na wenyeji za kiwango cha kikazi na sera zinazojumuisha uwiano wa HDP,** ili kupiga hatua na kuendeleza mbinu na mpango wa utekelezaji wa pamoja kati ya wafadhili, washirika, na mashirika ya wenyeji kote katika Muunganisho wa HDP.

# MAFUNZO

Msaada bora wa kibinadamu unajikita kwa mafunzo yanayoendelea, mbinu zilizojikita kwenye ushahidi, uwajibikaji, na uwezo wa kubadilika. Shirika la USAID linawekeza sana katika kujifunza na kujenga msingi wa ushahidi ili kuboresha hatua za uendeshaji zinazochukuliwa wakati wa hali ya dharura na ubora wa mpango wa kiufundi ili kutoa msaada kwa wakati unaofaa, kwa kuzingatia muktadha na kwa ufanisi. Juhudi za ujanibishaji zinahitaji kiwango hiki cha umakini kitumike katika kushughulikia changamoto za ushirikiano wa wenyeji, ikiwa ni pamoja na kupitia ukusanyaji na uchanganuzi wa kina wa mafunzo yaliyopatikana katika ushirikiano wa zamani na wa sasa. Kujumuisha na kuwasiliana kuhusu mchakato wa kujifunza na kutoa maoni katika michakato ya ujanibishaji kutajumuisha sauti za wenyeji na kuangazia na kusherehekea mafanikio ya sasa. Kutasaidia pia katika uwajibikaji wa washirika wenyeji na watu wanaowahudumia na kutambua fursa za kuboresha, kuhimiza uigaji wa tabia nzuri, mazungumzo mapana kuhusu makosa yanayoweza kutokea, na utatuzi wa matatizo kwa pamoja na ugavi wa rasilimali. Hatua hizi zinakubaliana na lengo la Sera ya LLHA juu ya uimarishaji wa uwezo wa ndani wa shirika la USAID pamoja na Agenda ya Mafunzo ya mwaka wa 2022-2026 ya shirika la USAID. USAID litaendelea kuwahusisha watu walioathirika katika kufuatilia na kutathmini mbinu za uingiliaji kati, ikijumuisha kutumia viashirio vya kawaida na vilivyowekwa katika muktadha ili kusaidia kupima ukubwa wa athari.

# HITIMISHO

Shirika la USAID litatumia Sera ya LLHA kuongoza jinsi inavyopanga shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu na jinsi Shirika litakavyofanya kazi katika miaka ijayo. Ofisi za shirika la USAID, Ofisi za Mashirika Huru na Misheni, pamoja na washirika wa utekelezaji wa shughuli za kutoa misaada ya kibinadamu, wana majukumu muhimu ya kutekeleza katika kuinua na kuboresha sauti, uwakilishi na uongozi wa watendaji na mashirika ya wenyeji ili kujenga mfumo wa kuchukua hatua wakati wa janga la kibinadamu ambao tunatazamia kuunga mkono. Kwa pamoja, mabadiliko haya yaliyofanywa kwenye mfumo yana uwezo wa kuboresha maisha ya watu walioathiriwa na janga duniani kote na kufikia maono ya pamoja ya shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji.

Kama mhisani mkubwa zaidi wa shughuli za kibinadamu duniani, shirika la USAID linapanga kutumia nafasi yake kushirikiana na wahisani wengine na mashirika mengine ya kibinadamu ili kuharakisha shughuli za kutoa msaada wa kibinadamu zinazoongozwa na wenyeji. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu walio katika hatari, iwe ni kwa sababu ya athari za mabadiliko ya tabianchi au dharura changamano za muda mrefu, shirika la USAID linasalia na nia thabiti ya kukabiliana na changamoto za kibinadamu za siku zijazo huku likichukua fursa za kukuza na kuunga mkono masuluhisho yanayoongozwa na wenyeji wakati wowote na popote inapowezekana.

# UFAFANUZI MUHIMU

**Uwezo** unajumuisha maarifa, ujuzi na motisha, pamoja na mahusiano yanaomwezesha mhusika—mtu binafsi, shirika au mtandao—kuchukua hatua ya kubuni na kutekeleza masuluhisho ya changamoto za maendeleo ya eneo husika na changamoto za kibinadamu, kujifunza na kujirekebisha kutokana na hatua hiyo na kuvumbua na kubadilka kadri muda unavyosonga.

**Kushiriki uwezo** ni mchakato wa kuimarisha ufanisi wa mtu binafsi na mfumo kupitia uwekezaji katika kubadilishana maarifa na kujenga ujuzi ambao unaweka kipaumbele katika mafunzo na ubadilishanaji wa pamoja kati ya wahusika, kwa kuzingatia utambuzi wa uwezo uliopo.

**Uimarishaji wa uwezo** ni uwekezaji wa kimkakati na wa makusudi katika mchakato wa kushirikiana na wahusika wa eneo husik—watu binafsi, mashirika, na watu mitandao—ili kuboresha kwa pamoja utendaji wa mfumo wa eneo husika kuzalisha matokeo ya kibinadamu na maendeleo yanayothaminiwa na wenyeji na yaliyo endelevu.

**Ufahamu wa masuala nyeti kuhusiana na migogoro** ni mazoea na mbinu inayolenga kuelewa mienendo ya muktadha dhahiri na isiyo dhahiri ili kuweza kuwa na uwezo wa kubadilika na kuchukua hatua dhidi ya mazingira changamano ya uendeshaji. Ufahamu wa masuala nyeti kuhusiana na migogoro unatambua kuwa hata uingiliaji kati wa maendeleo ulio na kusudi boro zaidi unaweza kuwa na athari mbaya na kuzidisha matatizo, lakini hutumia kanuni za Kuzuia Madhara na hutafuta kwa uangalifu kujenga miunganisho ya kijamii, kutafuta fursa zinazojenga amani na kukasuluhisha mivutano au migogoro.

**Uokoaji wa Haraka, Upunguzaji wa Hatari, na Ustahimilivu (ER4)** inaelezea kazi ya Ofisi ya Kutoa Msaada wa Kibinadamu ya shirika la USAID kuboresha ustawi wa watu wanaoishi katika mazingira hatarishi—kutoka kwa mtu binafsi hadi ngazi ya kitaifa—kwa kuimarisha uwezo wao wa kudhibiti hatari; kutarajia, kustahimili, kupona na kuendana na mishtuko na mifadhaiko; na kusaidia kuleta mabadiliko bora na makubwa.

**Makundi yaliyotengwa kihistoria** yanaweza kujumuisha, lakini sio tu, wanawake; vijana; watoto wanaokuzwa katika mazingira ya shida na familia zao; watu waliozeeka; watu wenye ulemavu; watu wa kikundi cha LGBTQI+; watu waliohamishwa kutoka kwa makazi yao; wahamiaji; Watu na jamii za Asili; makundi ya watu wachache wa dini fulani, rangi na makabila fulani; watu waliochukuliwa kuwa wa tabaka la chini tangu jadi; watu wa kiwango cha hali ya chini ya kijamii na kiuchumi; na watu wenye mahitaji ya afya ya akili ambayo hayajatibiwa.

**Hatua za kutoa msaada wa kibinadamu** ni kazi ya pamoja ya kuokoa maisha, kupunguza mateso, na kusaidia na kulinda watu wanaoishi katika mazingira hatarishi wakati na baada ya majanga.

**Uunganisho (Nexus) wa Shughuli za Kibinadamu-Maendeleo-Amani (HDP)** ni mbinu inayorejelea miunganisho kati ya shughuli za kibinadamu, maendeleo na amani kwa lengo la kuimarisha ushirikiano, mshikamano na usaidianaji. Mbinu ya Uunganisho (Nexus) wa HDP inalenga kutumia ubora wa kulinganisha wa kila nguzo—kwa kiwango cha umuhimu wake katika muktadha mahususi—ili kupunguza hatari ya jumla na idadi ya mahitaji ambayo hayajatimizwa, kuimarisha uwezo wa udhibiti wa hatari, na kushughulikia vyanzo vikuu vya migogoro. .

**Wahusika wa Eneo Husika** ni watu binafsi, mashirika, na mitandao ambayo yanatokana na kuongozwa na watu waliopo ndani ya nchi au eneo fulani ambalo ni mahali pao pakuu pa biashara au shughuli, ikijumuisha serikali katika viwango vya kitaifa na chini ya viwango vya kitaifa.

**Wahusika wa Eneo Husika,** kama inavyotumika katika Sera hii, inarejelea washirika wa eneo na wa kikanda, kama inavyofafanuliwa ndani ya mifumo ya shirika la USAID kama washirika waliojumuishwa na walioko katika nchi au eneo la mahali pao pa utendaji, mradi nchi ambapo mshirika alipo na kujumuishwa kwake si nchi yenye mapato ya juu kulingana na hifadhidata ya usambazaji wa mapato ya Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo.

**Ujanibishaji** ni seti ya mageuzi ya ndani, hatua zinazochukuliwa na mabadiliko ya tabia ambayo USAID inatekeleza ili kuhakikisha kuwa kazi ya Shirika inahakikisha kuwa inawapa uongozi wahusika wa eneo husika, kuimarisha mifumo ya eneo husika, na kusikiliza jamii za wenyeji.

**Usaidizi wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji** hutokea wakati wahusika wa eneo na kitaifa wanaongoza katika hatua moja au zaidi za kutoa msaada wa kibinadamu na/au hatua za ER4: utoaji wa bidhaa za matibabu ya dharura, tathmini ya mahitaji ya jumuiya, kufanya maamuzi, kupanga, uratibu, ugavi wa rasilimali, na ufuatiliaji na tathmini.

**Makundi yenye uwakilishi mdogo** ni yale ambayo yametengwa kwa kiasi kikubwa kutoka kwa fursa na mifumo (k.m., ajira, uwakilishi wa kisiasa, elimu, huduma za msingi), mara nyingi kutokana na vizuizi vya kimuundo na kijamii na kutengwa kihistoria.

# References


Babister, E. (2019). *Ownership and Participation in Local-Global Partnerships: The Recovery of Shelter and Settlement after Humanitarian Crises.* Journal of International Development. Volume 32, Issue 1.

Baguios, A. (2021). *Localisation Re-imagined: Fertilising the Soil of State-led Solutions.* ALNAP (Active Learning Network for Accountability and Performance in Humanitarian Action).

Barbelet, V., Davies, G., Flint, J., & Davey, E. (2021). *Interrogating the Evidence Base on Humanitarian Localization*. Humanitarian Policy Group Literature Review. ODI (formerly Overseas Development Institute).

Bhargava, Ruma & Bhargava, Megha (2023). *The Climate Crisis Disproportionately Hits the Poor. How Can We Protect Them?* World Economic Forum.

Dizolele, M.P., Kurtzer, J., & Abdullah, H.F. (2022). *Localizing Humanitarian Action in Africa*. Center for Strategic & International Studies (CSIS).

Fine, P. (2022). *Rethinking the Constraints to Localization of Foreign Aid.* Brookings Institution.

Foley, M. & Forsythe, K. (Editors). (2021). *Localisation and Local Humanitarian Action*. Humanitarian Exchange. Issue 79. Humanitarian Practice Network.

Juilliard, H. & Jourdain, J. (2019). *Lessons Paper: Responding to Earthquakes.* ALNAP.

Metcalfe-Hough, V., Poole, L., & Bailey, S. (2018). *Grand Bargain Annual Independent Report*. ODI (formerly Overseas Development Institute).

Robillard, S., Atim, T., & Maxwell, D. (2021). *Localization: A Landscape Report*. Tufts Feinstein International Center.

Stoddard, A., Czwarno, M. & Hamsik, L. (2019). *NGOs & Risk. Managing Uncertainty in Local-International Partnerships.* Global Report. InterAction and Humanitarian Outcomes.

Stoddard, A., Harvey, P., Timmins, N., et al. (2022) *Enabling the Local Response: Emerging Humanitarian Priorities in Ukraine, March-May 2022.* Humanitarian Outcomes.

**U.S. AGENCY FOR INTERNATIONAL DEVELOPMENT**
1300 Pennsylvania Avenue, NW, Washington, DC 20004
**T:** (202) 712-0000 | USAID.gov